

07-Adabu Za Kusoma Qur-aan

Kusoma Qur-aan ni *'ibaadah* miongoni mwa *'ibaadah* anazokusudiwa Allaah (سبحانه وتعالى) Pekee; hivyo basi *maqurraa-a* wa Qur-aan wamependekeza mambo au mapambo ambayo yanapendeza ajipambe nayo kila anaetaka kusoma Qur-aan. Miongono mwa yaliyopendekezwa ni:

1. Kuweka udhu, kwa sababu Qur-aan ni miongoni mwa *dhikru-Allaah* iliyo bora kabisa, japokuwa kisomo cha Qur-aan cha asiyekuwa na udhu kinajuzu.
2. Usafi na *twahaarah* ya nguo na mahali anapokaa kusoma kulingana na utukufu wa Qur-aan.
3. Kuelekea *Qiblah*.
4. Kuanza kwa *Isti'aadhah* na ma'ulamaa wengine wamewajibisha hili.
5. Kutoiacha *BismiLLaahi* mwanzo wa kila Suwrah isipokuwa *Suratut-Tawbah*.
6. Kuambatanisha *Isti'aadhah* na *BismiLLaahi* pale unapoanza Aayah zenye Majina ya Allaah (سبحانه وتعالى) na kutosoma *BismiLLaah* pale unapoanza na Aayah zenye kumtaja shaytwaan kuchunga kutoharibika kwa maana.
7. Kusoma kwa kutafakari na kuzingatia unachokisoma kama kwamba maneno ya Qur-aan unasemewa wewe kwani hili ndio kusudio na lengo kuu la kusoma Qur-aan; nako ni kufanya juu chini kuhakikisha kuwa moyo wako unashughulika na kuzingatia maana ya ukisomacho.
8. Kuisoma kwa utulivu, khushuu (unyenyekavu) wa kukhofu na kuheshimu maneno ya Mola Muumba, ambayo kama Anavyosema Mwenyewe (سبحانه وتعالى)

لَوْ أَنْزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَى جَبَلٍ لَرَأَيْنَاهُ خَشَعًا مُتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ

((Lau Tungeliiteremsha hii Qur-aan juu ya jabali, ungeliliona linanyenyekoa (na) lenye kupasukapasuka kutokana na khofu ya Allaah.))¹

9. Kuisoma kwa *tartiyl*: Kuipa kila herufi haki zake inazostahiki kama kilivyokuwa kisomo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kama ilivyothibiti katika Hadiyth ya Anas bin Maalik (رضي الله عنه) alipoulizwa kuhusiana na kisomo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) alijibu kwa kusema: "**Kisomo chake kilikuwa cha kuvuta, kisha akasoma: BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym: Akirefusha 'Allaah', na kurefusha 'Ar-Rahmaan', na kurefusha 'Ar-Rahiym**². Kupendezesha sauti yako kwani sauti nzuri ina athari zake katika nafsi ya msomaji mwenyewe na msikilizaji.
10. Kuathiriwa na Qur-aan, kwa kuomba kinga ya moto na adhabu, au kuomba maghfirah, Rehma, *Jannah* n.k. kila unapopitia Aayah zinazotaja hayo.
11. Kuathiriwa na Qur-aan, kwa kuhuzunika na kulia kwa kuguswa na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى). Kulia kwenye Aayah zenye kutaja adhabu, kwa kujifikiria ulichokiacha au *kukiqassir* (kukipunguza).
12. Kutokukatiza kusoma kwa ajili ya kuzungumza na watu au kuitikia salaam ila ikihitajika.
13. Kusujudu katika Aayah zenye alama ya *sijdah*.
14. Kunyanyua sauti pale inapokuwa kuinyanyua ni bora isipokuwa ikiwa utakhofia *riyaa-a* (kujionyesha), au kuwashawishi wenye kuswali, basi kusoma kwa sauti ya chini wakati huu itakuwa bora kabisa.

¹Al-Hashr (59: 21)

²Al-Bukhaariy